


# UQAB
Jarida la

Toleo 18 - Shawaal 1439 AH / Julai 2018 Miladi



**Idadi Kubwa ya Wafungwa wa Kisiasa Nchini Urusi ni Mashabab wa Hizb ut Tahrir!**

**Miito ya Kura ya Maamuzi Yathibitisha Kuwa Sheria Zilizotungwa na Mwanadamu Zaweza Kubadilishwa**

**Tumcheni Mwenyezi Mungu (swt) kikamilifu**

**Kuangazia Safari ya Mtume (saw) Kwenda Taif**

**Njia ya Mtume (saw) Kuleta Mageuzi - Halaqa 14**

**SWALI/JAWABU: Trump Kujitoa katika Makubaliano ya Nuklia**




## Kifungo cha Watoto Wahamiaji chaTrump Chadhihirisha Umbile la Kinyama Lisilokubalika la Nidhamu ya Kitaifa ya Kidemokrasia ya Amerika

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَٰنِ الرَّحِيمِ

Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir

﴿وَعَدَ اللَّهُ الَّذِينَ آمَنُوا مِنكُمْ وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ لَيَسْتَخْلِفَنَّهُمْ فِي الْأَرْضِ كَمَا اسْتَخْلَفَ الَّذِينَ مِن قَبْلِهِمْ وَلَيُمَكِّنَنَّ لَهُمْ دِينَهُمُ الَّذِي ارْتَضَىٰ لَهُمْ وَلَيُبَدِّلَنَّهُم مِّن بَعْدِ خَوْفِهِمْ أَمْنًا يَعْبُدُونَنِي لَا يُشْرِكُونَ بِي شَيْئًا وَمَن كَفَرَ بَعْدَ ذَٰلِكَ فَأُولَٰئِكَ هُمُ الْفَاسِقُونَ﴾

حزب التحرير
Hizb ut Tahrir

KUMB: 28/1439 | Ijumapili, 10 Shawwal 1439 H | 24/06/2018 M

# Kifungo cha Watoto Wahamiaji chaTrump Chadhihirisha Umbile la Kinyama Lisilokubalika la Nidhamu ya Kitaifa ya Kidemokrasia ya Amerika

**Taarifa kwa Vyombo vya Habari**

Chini ya sera ovu ya uhamiaji ya 'kutokuwa na hata chembe ya uvumilivu' ya Raisi wa Amerika, takriban watoto 2000, wengine wao wakiwa na umri mdogo wa miaka 4 au 5, ni miongoni mwa wale walioorodheshwa kama 'wahamiaji haramu', wametenganishwa kwa nguvu kutoka kwa wazazi wao katika mpaka wa Amerika na Mexico katika kipindi cha wiki sita pekee. Wametiwa ndani ya vibanda vya seng'enge katika vituo vya vizuizi, ambavyo hali zake zimesifiwa kuwa 'mithili ya gereza'. Mojawapo ya vituo hivi vya wahamiaji katika jimbo la Texas kimepewa lakabu ya La Perrera, "kibanda cha mbwa", ambamo watoto wanalala chini sakafuni juu ya magodoro membamba na makaratasi ndio blanketi zao. Kanda ya sauti ya watoto walioathirika kimawazo na kulia imepatikana, wakililia wazazi wao. Idara zimetangaza mipango ya kujenga mahema yatakayobeba mamia zaidi ya watoto katika jangwa la Texas ambako viwango vya joto kawaida hufikia nyuzi 40.

Licha ya kudhihirishwa hasira na shutuma kutoka kwa wanasiasa wa Amerika, vyombo vya habari vya kimagharibi na hata wake za waliokuwa maraisi dhidi ya unyama wa Trump kwa watoto hawa wahamiaji, wamepuuzia kimakusudi ukweli kwamba ni nidhamu katili ya kitaifa ya kidemokrasia ya Amerika ndiyo iliyoruhusu kanuni ya Flores dhidi ya kutoa makao kwa uhamiaji ambayo nyuma ilipitishwa na bunge la Congress inayohalalisha kwa kuruhusu idara kuwatenganisha watoto kutoka kwa wazazi wao kwa njia hii ya kinyama. Hivyo basi sera hii 'isiyokubalika' sio tu natija ya ukatili wa Raisi pekee. Ni mojawapo ya matunda yaliyooza ya nidhamu 'isiyokubalika' ya kidemokrasia ya Amerika inayofungua mlango kwa sera ovu kama hii inayopitishwa na kuidhinishwa na sheria, kwa msingi uchukizao wa ubaguzi wa kitaifa wa wale wanaotawala. Ni dalili gani zaidi inayohitajika kudhihirisha unyama huu wazi, upuzi na ubaguzi wazi wa rangi wa utaifa na muundo wa siasa za kitaifa za dola, unaodunisha, kudhalilisha, kunyanyasa na kutesa watoto wa wale ambao haja yao ni kutafuta tu maisha bora ya kiuchumi kwao na familia zao, lakini ikatokea kuwa wamezaliwa katika ardhi tofauti? Trump hajutii kuwaita wahamiaji kama wanaoleta "vifo na uharibifu" nchini na kama "wezi na wauwaji", akijua kuwa hakuna hatua za kisheria atakazochukuliwa kutokana na matamshi yake maovu, ya uchochezi, na ya ubaguzi wa rangi. Ule ukweli kuwa dola yenye uchumi imara ulimwenguni na ardhi kubwa, kuwakataza majirani zake kuingia, kutokana na kuwatazama kama mzigo kwa uchumi, inaeleza kwa kinywa kipana kuhusu roho mbaya, na umbile la uchoyo la mfumo wa kimada wa kirasilimali na siasa zake za dola za kitaifa zilizofeli kwa wanadamu. Tumeshuhudia pia unyama sawa na huu na misimamo ya kikatili dhidi ya uhamiaji iliyochukuliwa na mataifa ya kirasilimali ya Ulaya, Australia na ulimwengu wa Kiislamu – ambako watu wenye fadhaiko wanaokimbia mateso na unyama wamenyimwa hifadhi, wamefanyiwa idhilali ya hali ya juu na kuregeshwa kwenda kufa katika maeneo ya vita au kutelekezwa kufa maji baharini, yote ikiwa tu ni kwa sababu ni watu wenye utaifa tofauti na ardhi wanakotafuta hifadhi.

Kinyume na nidhamu ya kitaifa ya kidemokrasia ya Amerika inayoonesha ulimwengu kuwa ndio kigingi cha unyama, Khilafah kwa njia ya Utume inapinga fahamu ya mipaka katili ya kitaifa pamoja na utaifa au uasabiya wa kila aina. Badala yake, itawakaribisha wale wanaotoka katika ardhi nyenginezo kuja kuishi chini ya utawala wake ili waonje uadilifu wa hali ya juu na ufanisi wa mfumo wa Allah (swt). Hii ndio sababu Khilafah ya nyuma ilitoa hifadhi kwa zaidi ya Mayahudi wakimbizi 150,000 waliokuwa wakikimbia mateso kutoka kwa Manaswara wakati wa uchunguzi wa Kihispania na kuwawezesha kunawiri chini ya utawala wa Kiislamu. Khalifah wa zama hizo, Sultan Bayezid II pia alituma maagizo katika kila sehemu ya dola kwamba wakimbizi hao wapokewe. Katika tangazo lake, Sultan huyo aliwaambia Mayahudi kuwa kuwachunga wao ni amri ya Allah, kuona kuwa wako na chakula na kuwaweka chini ya ulinzi wake. Yote haya yanaonesha tofauti baina ya nidhamu ambayo lengo lake ni kumnyanyua mwanadamu kutokana na unyanyasaji, kinyume na nidhamu ambayo ufafanuzi wake wa ubora ni kuulazimisha juu ya wanadamu!

**"Hakika Allah anaamrisha kufanya uadilifu, na ihsani, na kuwapa jamaa wa karibu; na anakataza uchafu (zinaa), na uovu, na dhulma. Anakupeni mawaidha ili mupate kukumbuka." [16: 90]**

**Dkt. Nazreen Nawaz**
**Mkurugenzi wa Kitengo cha Wanawake katika Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir**

# Idadi Kubwa ya Wafungwa wa Kisiasa Nchini Urusi ni Mashabab wa Hizb ut Tahrir!



**Habari:**

Mnamo 14 Juni mtandao wa IA "Memo.ru" uliripoti: "Huku Kombe la Dunia likielekea kufanyika nchini Urusi, "Memorial" ilichapisha orodha ya wafungwa wa kisiasa. Orodha ya wale walioteswa kuhusiana na kupatikana kwa haki ya uhuru wa kuabudu na kujinasibisha na dini ilikuwa kutoka watu 97 mpaka watu 108. Idadi kubwa ya wale ambao majina yao yalikuwemo ndani ya orodha hii wanatuhumiwa kushiriki ndani ya harakati ya "Hizb ut Tahrir al-Islami", iliyotangazwa kuwa ya kigaidi nchini Urusi pasi na ushahidi wowote – hawa ndio walioshtakiwa katika kesi mbili jijini Moscow na Bashkortostan; Aidar Aydarbekov, Radik Imangulov, Sukhrob Ironov, Mirzobahovaddin Kurbonov, Nail Miniakhmetov, Akmalchon Numonchonov, Maxim Puigin, Naimjon Khodzhaev, Albert Shafiev; na Nariman Memedeminov, mwanaharakati wa Kitartari wa Crimea aliyetuhumiwa kwa kesi sawa na hii. Kuna watu wapatao 158 katika orodha tunazozichapisha leo: 50 kati yao wamo ndani ya orodha jumla ya wafungwa wa kisiasa, 108 – wamo ndani ya orodha ya watu walionyimwa uhuru wao kuhusiana na kupata haki ya uhuru wa kuabudu."

**Maoni:**

Kuna Mashabab 237 ambao kwa sasa wamenyimwa uhuru kutokana na kesi za Hizb ut Tahrir kwa jumla katika orodha ya Memorial. Katika orodha hio kuna wanawake pia. Mashabab wanahukumiwa vifungo visivyo na masharti vya muda mpaka wa miaka 19 gerezani. Leo, Mashabab 20 wanahukumiwa mjini Bashkiria. Kiongozi wa mashtaka ametaka Mashabab hawa wahukumiwe miaka 25 gerezani na faini ya ruble elfu 500.

Urusi katili wa muda mrefu imekuwa ikijiorodhesha kama adui wa Uislamu na Waislamu. Tukiiangalia historia kwa haraka, tutaliona hilo, tangu karne ya 16, kiongozi muovu, Tsar Ivan, alizinyakua ardhi za Waislamu – Kazan, Astrakhan na Siberia Khanates. Walipoteka miji, makatili hawa hawakuwasaza wanawake, wazee, wala watoto; walivamia miji na kuuwa maelfu ya Waislamu.

Kampeni za kijeshi za makatili hawa katika ardhi za Waislamu ziliendelea katika karne za 17-18, haya yalitokea katika Caucasus. Karne ya 19 iligubikwa na vita dhidi ya Khilafah ya Kiuthmani. Udikteta mpya ulioundwa wa ukomunisti mwanzoni wa karne ya 20 ndani ya Umoja wa Jamhuri Huru za Kisovieti (USSR), juu ya msingi wa fikra ya mada, uliendeleza vita dhidi ya Uislamu na Waislamu katika eneo la Asia ya Kati. Baada ya Vita vya Pili vya Dunia, serikali ya makafiri wa kikomunisti ilitekeleza ufurushaji mkubwa wa Waislamu Crimea na Caucasus. Matartari wa

*Endelea Uk..4*

Crimea, wachechnia, Waingush, Wadagestani wote walipelekwa eneo la Asia ya Kati. Katika eneo la Asia ya Kati lenyewe, maelfu ya Waislamu waliuwawa, wakiwemo wengi wa maulama wa dini na wasomi.

Sera hii ya chuki kwa Uislamu na Waislamu inaendelea hadi leo. Idara zinawatesa Waislamu wa Urusi kwa ukatili maalumu wa hali ya juu, hususan Mashabab wa Hizb ut Tahrir. Ili kumkamata Shab mmoja wa Hizb ut Tahrir utawala huu wa kinyama hutuma takriban polisi 20 waliojihami kwa silaha kochokocho wakivalia sare maalumu na viziba uso. Hakuna utawala wa nchi yoyote nyengine huituhumu Hizb ut Tahrir kuwa harakati ya kigaidi, isipokuwa idara za Urusi. Hakuna idara katika nchi yoyote nyengine ulimwenguni inayoweza kupitisha hukumu juu ya Mashabab wa Hizb ut Tahrir ya kuanzia miaka 15 hadi 20 gerezani. Hii ni ishara kuwa utawala wa kinyama wa Urusi inauogopa Uislamu na neno la haki kutoka kwa Mashabab wa Hizb ut Tahrir!

Hivyo basi, msimamo wa Waislamu kuhusiana na utawala katili wa Urusi unapaswa kuwa wazi na wa kukatikiwa. Waislamu wanakabiliana na adui kwa sura ya serikali ya Urusi, ambayo inawatesa Waislamu sio tu nchini Urusi pekee, bali pia nchini Syria, Asia ya Kati na sehemu nyenginezo ulimwenguni.

Ukombozi wa Waislamu wa Urusi, Asia ya Kati na nchi nyenginezo kutokana na uadui wa kinyama wa idara za Urusi uko kwa sura ya kipenzi chetu Mtume Muhammad (saw), nao ni, kurudisha tena dola ya Khilafah Rashida kwa njia ya Utume. Haya ni mapambano ya kimfumo na ya kisiasa pamoja na Hizb ut Tahrir dhidi ya serikali za madhalimu na makafiri.

Kwa kurudisha tena dola tukufu, Khilafah, inayoongozwa na mtawala mwema, Waislamu watapata ngao itakayowalinda Waislamu wote duniani kutokana na mateso ya wakoloni makafiri na vibaraka wao, usoni mwa watawala fisidifu wa Waislamu. Kama alivyosema kipenzi chetu Mtume Muhammad (saw):

«إنما الإمام جنة يقاتل من ورائه و يتقى به»
“Hakika Imam ni ngao, nyuma yake watu hupigana na kujilinda.” Hadith hii imesimuliwa na Imam Muslim.” Na twamuomba Allah atunusuru.

**Eldar Khamzin**
**Mwanachama wa Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir**

# Miito ya Kura ya Maamuzi Yathibitisha Kuwa Sheria Zilizotungwa na Mwanadamu Zaweza Kubadilishwa Kulingana na Maslahi ya Dola za Kikoloni



**Habari:**

Vyombo vya habari nchini Kenya vimesheheni ripoti za siasa za mgawanyiko juu ya kadhia ya ima tuwe na kura ya maamuzi au la. Kifiniko hiki cha kura ya maamuzi kilifunuliwa na Bwana Kassait Kamket, mbunge wa KANU anayejulikana kwa uchache kutoka Kaunti ya Baringo eneo bunge la Tiaty, aliyeuandaa mswada unaotafuta kubadilisha muundo wa utawala kutoka kuwa ni muundo wa ki-uraisi mpaka kuwa ni muundo wa ki-bunge. Kwa upande mwengine, tuna Raila Odinga (kiongozi wa ODM) na washirika wake wanaounga mkono hilo huku Naibu wa Raisi William Ruto na washirika wake wakipinga vikali hilo.

**Maoni:**

Baada ya Vita vya Pili vya Dunia, vilivyopelekea kuporomoka kwa utawala wa kiulimwengu wa Uingereza kutokana na kukumbwa na hali mbaya sana ya kiuchumi kwa kushiriki kwake katika vita hivyo. Iliamua kuzitawala koloni zake kwa njia isiyo ya moja kwa moja huku ikitulizia makini juu ya sera ya kindani, ambayo ilikuwa ikiyumba kutokana na udhaifu wa kiuchumi. Hii ilipelekea kuzuka kwa watawala vibaraka wa kikoloni wa Kiingereza katika koloni zake zote, waliojivisha guo la wazalendo, wanamapinduzi na mashabiki wa ukombozi dhidi ya utawala wa wazungu. Kenya kama dola ya kisekula ya kikoloni, iliyokuwa chini ya utawala wa moja kwa moja wa Uingereza kwa zaidi ya miongo sita ilipewa ‘bendera ya uhuru’ bandia iliyopelekea mamilioni ya Wakenya kusherehekea kwa furaha kwa kujitawala wenyewe (utawala wa weusi). Tahamaka! Walipata mshtuko mkubwa kwani ilikuwa ni mabadiliko ya sura tu lakini mfumo wa kisekula wa kikoloni na nidhamu zake ulikuwa ukitabikishwa juu yao ila wakati huu na wananchi wenzao ambao hawakuwa isipokuwa ni watawala vibaraka watiifu kwa wanaotumikia ufalme huo kwa gharama zote juu yao.

Amerika kwa upande mwengine, baada ya Vita vya Pili vya Dunia iliibuka kuwa yenye nguvu katika ulingo wa siasa za kiulimwengu. Hivyo basi, ilichukua fursa ya kudidimia kwa ushawishi wa Uingereza na kuongoza ajenda ya kiulimwengu dhidi ya koloni za Uingereza ili kuzinyakua na kuzitia katika kambi yake. Nchini Kenya, kampeni ya Kiamerika iliongozwa na Jaramogi Oginga kisha baadaye kuongozwa na mwanawe Raila Odinga na katika kambi ya Uingereza iliongozwa na Jomo Kenyatta, Daniel Moi, Mwai Kibaki na sasa Uhuru Kenyatta. Tangu wakati huo, mvutano wa kisiasa wa Kenya umebakia baina ya hao walioko katika kambi ya Amerika na kambi ya Kiingereza.

Kiasi ya kuwa kura zote za maamuzi na mabadiliko ya kikatiba yaliyoshuhudiwa nchini Kenya yalianzishwa na ima kambi ya Kiamerika au kambi ya Kiingereza kwa ajili ya maslahi yao kupitia viongozi vibaraka wao. Kambi hizi ima ziliidhinisha au kupinga mabadiliko wazi wazi baada ya

Endelea Uk..6

kuhakikishiwa kuwa vyeo vyao viko imara na kwamba mabadiliko hayo hayataathiri hali halisi iliyopo. Ndio maana si ajabu miaka hamsini na tano baada ya 'uhuru bandia', Wakenya wangali wanateseka na umasikini mkubwa, ukosefu wa ardhi na makao, viwango vya kushtua vya ukosefu wa ajira, kuporomoka kwa sekta za elimu na afya nk. Kwa sababu tangu mwanzoni mvutano wa kisiasa haukuwahusu wao Wakenya, bali wao walikuwa ni vikaragosi tu vya kisiasa vilivyotumiwa kama ngazi za vibaraka wabinafsi kubakia (Uingereza) au kuingia (Amerika) mamlakani. Kufafanua hili zaidi natoa yafuatayo:

**Baadhi ya Mabadiliko ya Kikatiba Yaliyofanywa (Yakisukumwa) na Wale Walioko Katika Kambi ya Kiingereza Ili Kudumisha/Kubakia Mamlakani:**

1. 1963 – Katiba ya uhuru wa Kenya ya mwaka wa 1963 inaruhusu mfumo wa vyama vingi. Jomo Kenyatta anatawazwa kama Waziri Mkuu wa kwanza wa Kenya.
2. 1964 – Kenya inakuwa jamhuri na Jomo Kenyatta anakuwa Raisi wa kwanza wa Kenya, huku cheo cha Waziri Mkuu kikifutiliwa mbali.
3. 1966 – Mabunge ya mikoa yanafutiliwa mbali. Bunge la Seneti linavunjwa na wanachama wake kuunganishwa na wale wa Bunge la Wawakilishi na kuwa Bunge moja kuu la kitaifa.
4. 1969 – Katiba mpya inatabanniwa, inayotilia nguvu marekebisho ambayo tayari yashafanyiwa katiba ya uhuru ya 1963, na kuyapa nguvu zaidi mamlaka ya raisi.
5. 1982 – Mfumo wa vyama vingi unapigwa marufuku na kuifanya Kenya kuwa dola ya chama kimoja huku KANU kikiwa ndio chama tawala. Hii ilifuatiwa na mfumo wa kura ya mlolongo ambapo kura za siri hazikutumika tena.
6. 2005 – Nakala ya katiba kielelezo ya Wako (iliitwa jina la Mkuu wa Sheria, Amos Wako) – iliyo orodheshwa na serikali badala ya nakala ya Bomas, iliyoikataa. Nakala iliyoboreshwa ya katiba ya 1969 lakini ikaondoa matakwa ya asilimia 25% katika chaguzi kuu ambayo yanamhitaji mshindi wa kura za uraisi kuwa na asilimia 25% ya kura kwa uchache katika mikoa mitano. Mshindi huyo pia atahitaji kupata zaidi ya asilimia 50% ya kura hizo zote, vyenginevyo kufanyika marudio ya hapo kwa hapo ya uchaguzi.

**Baadhi ya Mabadiliko ya Kikatiba Yaliyofanywa (Yakisukumwa) na Wale Walioko Katika Kambi ya Kiamerika ili Kuingia/Kupata Fursa ya Kutawala:**

1. 1991 – Raisi Moi mnamo Disemba 1991 katika mkutano wa wajumbe wa KANU katika uga wa Kasarani, alifutilia mbali sehemu ya 2A ya katiba, hivyo basi kuifanya Kenya kuwa dola ya vyama vingi. Mabadiliko hayo yaliingiza kuwepo kwa mihula ya kuhudumu ya raisi.
2. 2000 – Tume ya Kurekebisha Katiba ya Kenya yaundwa na Raisi Moi na Profesa Yash Pal Ghai kuwekwa kama mwenyekiti wake kuongoza mageuzi ya kwanza makuu ya katiba ya Kenya.
3. 2004 – Nakala ya Bomas (iliyopewa jina la eneo ambalo kongamano la mageuzi ya katiba lilifanyika na kuitabanni) – iliyopendekeza kuhamisha mamlaka mengi ya afisi ya Raisi aliyechaguliwa na watu na kuyapeleka kwa Waziri Mkuu ambaye atachaguliwa na Bunge. Zaidi ya hayo, kungekuweko na uangalizi na kuhisabiwa kwa teuzi za mawaziri. Waziri Mkuu angependekeza wabunge kuwa mawaziri, na kisha Raisi angewateua. Teuzi zote zingehitaji kura za maseneta.
4. 2005 – Mnamo Novemba 2005, kura ya maamuzi ya katiba yalishinda pendekezo la serikali la katiba mpya.
5. 2008 – Mnamo Machi 2008, Bunge la Kitaifa la Kenya lapitisha kifungu cha sheria cha Uwiano wa Kitaifa kilicholeta mabadiliko ya muda kwa katiba kwa kubuni cheo cha Waziri Mkuu na Manaibu Waziri Mkuu wawili.
6. 2009 – Bunge layapa kipaumbele mageuzi ya katiba kupitia Ajenda Na. 4 juu ya namna mageuzi haya yatakavyo fanywa itajadiliwa katika kikao cha pili cha Bunge la kumi lililoanza mnamo Aprili 2009.
7. Agosti 2013 – Katiba kielelezo yaidhinishwa na kiwango cha asilimia 67% katika kura ya maamuzi ya kitaifa. Katiba mpya yatangazwa rasmi mnamo 27 Agosti.

Kwa kutamatisha, kwa kadri ya idadi ambazo Wakenya watakwenda katika kura za kuleta mabadiliko ya kikatiba. Tatizo msingi linalowakabili wao ni utabikishwaji wa mfumo wa kisekula wa kirasilimali na nidhamu zake ikiwemo ya kijambazi ya demokrasia, uhuru wa kijamii, nidhamu dhalimu ya kiuchumi nk kutawala mambo yao ya kimaisha. Usekula umechipuza kutokana na akili finyo ya mwanadamu kwa msingi wa maslahi, hamu na matamanio. Suluhisho ni kubadilisha mfumo wa kisekula wa kirasilimali na kukumbatia Ulinganizi wa Mwamko wa Kiislamu wa Kiulimwengu. Ulinganizi wa kihakika unaolenga kuwakomboa wanadamu ulimwenguni kutokana na njama za wakoloni wa kimagharibi na mfumo wao batili wa kisekula wa kirasilimali na nidhamu zake. Ulinganizi wa mwamko ambao kilele chake ni kulingania kusimamishwa tena kwa Khilafah (Dola ya Kiislamu) kwa njia ya Utume katika nchi yenye idadi kubwa ya Waislamu. Kuanzia hapo, nchi hiyo yenye idadi kubwa ya Waislamu itakuwa ndicho kitovu cha kuwaunganisha wanadamu ulimwenguni chini ya Khalifah mmoja mwadilifu (Kiongozi wa Dola ya Kiislamu) anayetawala kwa Qur'an, Sunnah, Ijmaa' Sahaba na Qiyas.

**Ali Nassoro Ali**
**Mwanachama wa Afisi ya Habari ya Hizb ut Tahrir Kenya**

*Endelea Uk..8*

# Maisha haya ya dunia si chochote bali ni mafupi, kwa hiyo Tumcheni Mwenyezi Mungu (swt) kikamilifu

Uendaji mbio, uchangamfu, uchukuliaji mambo kwa udharura na upangaji mipango na ufuatiliaji katika kufanya da'wah tuliouona katika maisha ya Mtume (saw) ilikuwa sio eti ana "dhibiti wa wakati". La, ilikuwa ni athari ya kukatikiwa juu ya maisha haya ya dunia, kama ilivyo pambanuliwa katika yale ambayo Mwenyezi Mungu (swt) aliyoyaeleza. Hakika, uhai umedhihirishwa kuwa ni mfupi,hata na wale ambao wameishi muda mrefu miongoni mwa watu.

Mwenyezi Mungu (swt) alisema:

وَلَقَدْ أَرْسَلْنَا نُوحًا إِلَىٰ قَوْمِهِ فَلَبِثَ فِيهِمْ أَلْفَ سَنَةٍ إِلَّا خَمْسِينَ عَامًا فَأَخَذَهُمُ الطُّوفَانُ وَهُمْ ظَالِمُو

"Na hakika tulimtuma Nuhu kwa watu wake, na akakaa nao miaka elfu kasoro miaka hamsini, Basi tufani liliwachukua, nao ni madhalimu." [Al-Ankabut: 14]

Mtume (saw) alisema:

**"Malaika wa mauti alikuja kwa Nuhu (as) na kumuuliza: Ewe Nuhu, Mtume uliyeishi miaka mingi zaidi, uliyaonaje maisha haya ya dunia na starehe zake? Akajibu: Ni kama mtu niliyeingia katika chumba kilicho na milango miwili, na nikasimama katikati ya chumba kwa muda mfupi, kisha nikatoka kwa mlango mwengine"** Huo ndio mtizamo wa Nuhu (as) aliyeishi karne tisa na nusu, je, sisi tuyatizame vipi maisha yetu Ummah wa Muhammad (saw); ambayo Mtume (saw) alisema:

**"Maisha ya Ummah wangu ni kuanzia miaka sitini hadi sabini."** [Tirmidhi]

Je sisi sio kama ambao tunazaliwa karibu na mlango tunaotakiwa kutoka? Au sio hivyo? Je kweli tunayo maisha ya kutosha kiasi kwamba tucheleweshe kuiendea mbio Dini yetu? Ni jukumu la kila mmoja wetu kwenda mbio kuhakikisha kuwa umri wake haukupotea bure. Kila siku na kila sehemu ya siku yetu lazima ihesabike kwa kuishi maisha yanayomridhisha Mwenyezi Mungu (swt).

Hakika maisha haya ya dunia si chochote bali ni mafupi na Siku ya Kiyama, yatakumbukwa hivyo na wale ambao hawakumcha Mwenyezi Mungu (swt). Watakuwa wameumaliza umri wao katika michezo na kuyakimbilia matamanio yao. Watakuwa katika waliokata tamaa kutokana na kuumaliza uhai wao na watadai kuwa umri wao ulikuwa ni siku moja au sehemu ya siku.

Mwenyezi Mungu (swt) alisema:

"**Mwenyezi Mungu Atasema: Mlikaa muda gani katika ardhi kwa hisabu ya miaka? Watasema: Tulikaa siku moja au sehemu ya siku. Basi waulize wanao weka hisabu. Mwenyezi Mungu Atasema: Nyinyi hamkukaa huko duniani ila kidogo, laiti ingeli kuwa mnajua. Je! Mlidhani ya kwamba tulikuumbeni bure na ya kwamba nyinyi kwetu hamtarudishwa? Ametukuka Mwenyezi Mungu, Mfalme wa Haki, hapana mungu ila Yeye, Mola Mlezi wa A'rshi Tukufu**." [Al-Muminun: 112 -116]

Hivyo tunatakiwa kuzitumia vipi siku au sehemu ya siku zetu? Kwa kipimo kipi tunatathmini kuwa siku nzima iliyotumika kuwa na familia, au kukaa afisini hadi usiku sana kwamba ni kuutumia vyema muda; lakini masaa kadhaa kuyatumia katika kazi ya kulingania kusimamisha Khilafah kwa Njia ya Utume kwamba ni muda uliopotea? Tunawezaje kupumzika majumbani mwetu siku yoyote au sehemu ya siku ilhali Dini ya Mwenyezi Mungu (swt) haitekelezwi, damu ya Waislamu inanyunyizwa katika ardhi, ardhi za Waislamu zimevamiwa na watu duni katika binadamu na Waislamu wametawanyika katika ulimwengu kama wakimbizi, wakizama baharini wakimbia au wakilala peupe kwenye baridi na bila chakula? Je ni kweli tunao muda wa kupumzika na je, huu ni muda wa kupumzika?

Tusikubali kudanganywa na shetani kuhusu kuwepo kwetu hapa duniani. Si tu kwamba maisha haya ni mafupi bali kwa hakika ni mafupi ukilinganisha na ya Akhera yenye kudumu.

Mwenyezi Mungu (swt) alisema:

وَمَا الْحَيَاةُ الدُّنْيَا فِي الْآخِرَةِ إِلَّا مَتَاعٌ

"...**Na uhai wa dunia kwa kulingana na Akhera si kitu ila ni starehe ndogo.** [Ar-Rad 13: 26]

Mwenyezi Mungu (swt) alisema:

قُلْ مَتَاعُ الدُّنْيَا قَلِيلٌ

"Sema: Starehe ya dunia ni ndogo." [An-Nisa' 4:77]

Mwenyezi Mungu (swt) alisema:

يَا قَوْمِ إِنَّمَا هَٰذِهِ الْحَيَاةُ الدُّنْيَا مَتَاعٌ وَإِنَّ الْآخِرَةَ هِيَ دَارُ الْقَرَارِ

"Enyi watu wangu! Hakika haya maisha ya dunia ni starehe ipitayo tu, na hakika Akhera ndiyo nyumba ya daima." [Ghafir: 39]

Mtume (saw) alisema:

**"Kwa Jina la Mwenyezi Mungu, hii dunia (si chochote ukiilinganisha) na Akhera ni kama mmoja wenu akitie kidole chake katika bahari na kisha akitoe aangalie kilichobakia kidoleni mwake."** [Muslim]

Hivyo basi, kwa nini tuiache bahari kwa kile kisichojaza hata kidole, tukienda mbio kwa masaa, masiku, mawiki na miezi? Tusipoteze muda kwa vitu ambavyo havina maana ambavyo vitatupelekea kutoshughulikia matendo ambayo tumeamrishwa juu yetu. Hakika, lazima tuchunge wakati tukiiendea mbio dunia kila dakika, saa na siku ili tuweze kupata nafasi ili kufanyiakazi yale mambo muhimu kuhusiana na Akhera yenye kudumu.

Sio tu kwamba maisha ya dunia ni mafupi bali pia yanaweza kuisha wakati wowote. Hakuna kuepuka au kukimbia kifo. Wakati wa kifo hatuujui sisi, sasa iweje kuhairisha kile ambacho Mwenyezi Mungu (swt) ametuamrisha? Kuhairisha huko

*Endelea Uk..8*

kumejengwa juu ya kujidanganya binafsi, matumaini ya kirongo na mtizamo finyo.

Mwenyezi Mungu (swt) alisema:
وَلِكُلِّ أُمَّةٍ أَجَلٌ فَإِذَا جَاءَ أَجَلُهُمْ لَا يَسْتَأْخِرُونَ سَاعَةً وَلَا يَسْتَقْدِمُونَ
"Utakapofika muda wao basi hatakawia hata saa moja, wala hawatatangulia." [Al-Aa'raf 7:34]

Mtume (saw) alisema:
**"Kila mara kumbuka muuaji wa furaha, akimaanisha kifo."** [Ibn Maajah]

Hatutakiwi kuchelewesha mambo ya Dini yetu kwa matumaini kuwa bado tutakuwepo mwezi ujao, wiki ijayo, kesho au hata saa ijayo. Matumaini hayo ni ya uongo. Hakika, mwanadamu hufikwa na kifo kabla matumaini hayo hayaja kamilika.

Mtume (saw) alichora mistari michache na kusema:
**"Haya ni matumaini ya mwanadamu, na haya ni mauti yake ghafla, na wakati yupo katika hali ya matumaini, ndivyo kifo kinavyomjia"** [Bukhari]

Tunawezaje kuupa mgongo mwito wa ulinganizi wa Khilafah ili kujiunga na kazi ya kusimamisha utawala kwa Shari'ah iliyoshukishwa na Mwenyezi Mungu (swt)? Tunawezaje kuhairisha juhudi muhimu za kusonga mbele katika kupambana na utawala wa kikafiri? Kwa nini ucheleweshe hadi kesho lile ambalo laweza kufanyika leo? Je hii sio kasi inayotakiwa kuwa nayo baada ya kuona kwamba twaweza kufa wakati wowote? Ikiwa hatuendi kwa kasi inayostahiki, je si lazima tubadilishe mazoea yetu ili tuweze?

Hakika maisha ya dunia ni mafupi, kwa hiyo tuyafanyie kazi vilivyo. Mipango, matamanio na furaha ya dunia hii yasitushughulishe na kuchukua muda wetu, kiasi kwamba hatuna nafasi iliyobakia kwa ajili ya kumuabudu Mwenyezi Mungu (swt) haki kamilifu.

Mtume (saw) alisema:
**"Ishi katika dunia hii kama ambaye ni mgeni au msafiri."** [Al-Bukhari]
Mwenyezi Mungu (swt) alisema:
أَرَضِيتُم بِالْحَيَاةِ الدُّنْيَا مِنَ الْآخِرَةِ فَمَا مَتَاعُ الْحَيَاةِ الدُّنْيَا فِي الْآخِرَةِ إِلَّا قَلِيلٌ
"Je, mmeridhia maisha ya dunia kuliko ya Akhera? Lakini starehe za maisha ya dunia kulinganisha nay a Akhera ni chache." [At-Tawba: 38]

Muislamu anaishi kama msafiri, anapita kupitia uhai, na haishi kama ambaye anaishi milele hapa. Hafikirii mara mbili kuhusu kubadilisha kazi lau inachukua muda wake ambao angelikuwa anafanya Da'wah au inayomchokesha kiasi kwamba haimpi nafasi ya kuwa katika uchangamfu kubeba Da'wah. Atapunguza mipango yake ya kuboresha biashara yake, kujiendeleza kiajira, kununua nyumba, kusomesha wanawe na kumfurahisha mkewe kwa sababu muda wake mwingi muhimu anautumia katika ulinganizi wa Uislamu.

Ukimuona utaona ishara ya ukosefu wa usingizi na mapumziko ndani ya mtu huyu. Licha ya hali hiyo, ukimuambia azidishe Da'wah, atakuwa tayari kufanya hivyo, kwa hiyari na bila kulalamika. Anafahamu fika uzito wa hotuba ya Mtume (saw) pale aliposema:
**"Hakuna kupumzika baada ya siku hii, Ewe Khadija."**

Ni yule anayekwenda mbio kwa malengo, bila kuhairisha au kusitasita kila anapojua kuna jambo la kufanywa kwa ajili ya Dini yake. Imesimuliwa na 'Uqba bin Al-Harith: Siku moja Mtume (saw) alipomaliza kuswali swala ya Asr aliondoka kwa haraka kuelekea nyumbani kwake na kurudi mara moja. Mimi (au mtu mwengine) tukamuuliza kuna tatizo gani na akajibu:
**"Nimewacha nyumbani kipande cha dhahabu ambacho kilikuwa ni cha Sadaka na sikupenda kibakie mpaka usiku katika nyumba yangu, hivyo nimeenda kukichukua nikigawanye"** [Bukhari]

Muislamu ni yule anayekimbilia bila kupoteza wakati katika kuendeleza ulinganizi wa mwito wa Mwenyezi Mungu (swt) hata kama ni hatari kwake yeye. Muslim amesimulia kuwa imeripotiwa kutoka kwa Ana b. Malik alisema: Mtume (saw) alimtuma Busaisah kama jasusi kuangalia msafara wa Abu Sufyan umefikia wapi… Washirikina wakawa wanatunyemelea na Mtume (Saw) akasema:
"**Inuka uingie Peponi ambayo upana wake ni sawa na mbingu na ardhi.**"
'Umair b. al- Humam al-Ansari alisema: "**Mtume wa Mwenyezi Mungu, Pepo ni sawa na urefu baina ya mbingu na ardhi**?" Mtume (saw) alisema"**Naam**." 'Umair alisema: "**Ubora ulioje!**" Mtume (saw) akamuuliza: "**Nini kilichokufanya utamke maneno hayo?** Akasema: **Mtume wa Mwenyezi Mungu,Si lolote bali ni hamu ya kuwa miongoni mwa wakaazi wake**" Mtume (saw) akamwambia: "**Hakika wewe ni miongoni mwa wakaazi wake**." Umair akatoa tende kutoka katika begi lake na kuanza kuzila. Kisha Umair alisema: "**Lau nitaendelea kuishi ili nile hizi tende zote zangu, itakuwa muda mrefu**. (Msimuliaji alisema): Alizitupa tende zote alizokuwa naz. Kisha akapigana na maadui mpaka akauawa." Hakika Muislamu hacheleweshi kujitoa muhanga hata kama ni kula mlo wake wa mwisho duniani.

Hakika maisha ya dunia hii si chochote bali ni mafupi na mwisho wake haujulikani na mtu yeyote, kwa hiyo tumcheni Mwenyezi Mungu (swt) kikamilifu. Lau tunazembea, tuzinduke kutoka katika kususuwaa hadi kufanya kazi. Ikiwa twatembea tuongeze kasi yetu. Tukamilishe mipango ya leo, leo, ili kesho tuzindue mipango mingine. Tuyafanye majukumu ya Dini na ya Ummah wetu yaamue kasi na sio kwamba majukumu haya yawachwe kutokana na kasi yetu. Twendeni mbio tukiwa wachangamfu na nishati ili umri wetu katika maisha haya mafupi yahesabiwe vilivyo wakati tutakaposimama mbele ya Mwenyezi Mungu (swt).

**Musab Umair – Pakistan**


Email: info@uqab.or.ke

# Kuangazia Safari ya Mtume (saw) Kwenda Taif



Katika mwezi wa Shawwal mwaka wa kumi wa Utume, aliondoka Mtume (saw) akifuatana na sahaba wake mtukufu Zaid bin Harithah kutoka Makkah kuelekea mji wa Taif kiasi cha maili 70 upande wa kusini mashariki. Dhamira ya safari hiyo ni kuomba nusra kutoka kwa viongozi wa kabila la Bani Thaqif wa mji wa Taif.

Nusra katika ulinganizi wa Mtume (saw) hukusudiwa uhamishaji wa hatamu na mamlaka ya kisiasa na kijeshi kwa kupitia kiapo maalum [baia] kinachotolewa na jopo la wenye nguvu au ushawishi katika jamii kwa lengo la kuondosha utawala uliopo na badala yake kuwezesha kusimamisha Dola ya Kiislamu.

Itakumbukwa kwamba baada ya ulinganizi wa Uislamu kuganda katika mujtamaa (jamii) wa Makkah, na kukataa kwao maQureshi kwa inadi na kibri dini ya Uislamu na kutokuwa tayari kusalimisha mamlaka yao kwa ajili ya kusimamisha Dola ya Kiislamu, ilimbidi Mtume (saw) kwa kuelewa kwamba ujumbe wake si wa kikabila au kizalendo kuja na mkakati wa kuyakabili makabila mengine nje ya Makkah ili kufanikisha lengo lake hilo.

Katika qadhia hii nyeti ya kutaka nusra Mtume (saw) alishika msimamo thabiti nao ni lazima wale anaowalingania kumpa nusra, waukubali Uislamu kwa ukamilifu wake na watoe mamlaka yao yote bila ya masharti yanayopingana na Uislamu ili Dola anayoikusudia kuisimamisha iwe Dola huru na sio tegemezi. Katika hilo alikuwa akiwaekekea wazi na bayana kwa makabila yote kwa kuyaeleza:

وأن تؤمنوا بي وتصدقوا بي وتمنعوني حتى أبيِّن عن الله ما بعثني به

"Ya kwamba mniamini, kunisadiki na kunilinda mpaka niweze kubainisha yale aliyonituma nayo Allah."
Makabila yaliupokea ulinganizi wake wa nusra kwa hisia tofauti. Kabila la Amir bin Sa'sa'ah walimueleza Mtume (saw) bayana msimamo wao kwa kuweka sharti la kuchukua wao utawala baada ya kuondoka Mtume (saw) nao walimjibu:

'Tuinamishe shingo zetu kwa panga za waarabu na mara ushindi ukipatikana utawala wende kwa wengine?' [Sira ya Ibn Hisham]

Kwa jibu hili ni wazi walielewa kwa kina upana na unyeti wa ajenda ya Mtume (saw) ya kuasisi Dola. Makabila mengine kama Bani Kinda na Bani Kalb yalimkatalia kimya kimya, ilhali Bani Hanifah walimkatalia kwa kudhihirisha uovu na ubaya dhidi yake (saw).

Safari ya Mtume (saw) kwenda Taif ilikuwa ni sehemu ya mchakato huo

Endelea Uk..10

wa kutafuta kuungwa mkono kufikia lengo lake tukufu, na mara baada ya kuwasili Taif alifanya hadhari kubwa kwa kuwakabili machifu watatu tu wa kabila la Bani Thaqif, nao ni mabwana Abd Yaliil, Masu'd na Habib wote wakiwa watoto wa Amr bin Umair At-Thaqafi ili kufikisha ajenda yake ya kuwataka wasilimu na watoe nusra yao kwake ili ahamie kwao na kusimamisha utawala wa Uislamu; na endapo hawatokubaliana na matakwa yake basi qadhia ile ibakie kuwa siri baina yao bila ya kudhihirishwa kwa yoyote.

Kwa bahati mbaya na kwa masikitiko makubwa, machifu wa kabila hili kama makabila mengine mengi hawakukubali matakwa ya Mtume (saw). Bali baya zaidi hawakuheshimu hata siri waliyoombwa kuihifadhi na badala yake si tu walivujisha siri ya mazungumzo yale, bali kwa kibri na inadi wakamtokomeza Mtume (saw) kwa watu waovu na wahuni waliompiga kwa mawe na kuimwaga damu yake tukufu kwa kebehi, dhihaka, bughdha na majivuno. Lakini Mtume (saw) alidumu na da'wa yake japo kuwa alisibiwa na mitihani kama jibu baya la machifu wa Banu Thaqif nk.
Mtume (saw) alirejea na kuingia tena Makkah kwa dhamana/kinga ya Mut'im bin Addiy akiwa amechoka na majeraha lakini hakuvunjika moyo, kuteteleka wala kurudi nyuma katika mchakato wa ulinganizi na kutafuta nusra mpaka makabila ya Aus na Khazraj ya Madinah yalipompa kiapo cha vita (baay'atul-harb) huku wakimueleza:

فَأَخَذَ الْبَرَاءُ بْنُ مَعْرُورٍ بِيَدِهِ ثُمّ قَالَ نَعَمْ وَاَلّذِي بَعَثَك بِالْحَقّ ( نَبِيّا ) لَنَمْنَعَنّك مِمّا نَمْنَعُ مِنْهُ أُزُرَنَا فَبَايِعْنَا يَا

رَسُولَ اللّهِ فَنَحْنُ وَاَللّهِ أَبْنَاءُ الْحُرُوبِ وَأَهْلُ الْحَلْقَةِ..

"Al-Bara bin Ma'aroor [Answari] akachukua mkono wake [mkono wa Mtume (saw)] kisha akasema: 'Naam naapa kwa Yule ambaye amekutuma kwa haki (kuwa Mtume) kwamba tutakulinda kama tunavyolinda wakaribu wetu. Basi ikubali bay'a yetu ewe Mtume wa Allah kwani sisi Wallahi ni watoto (yaani wazoefu) wa vita na watu wa kupigana kwa mzunguko."

Kwa nusra aliyopewa na Answar, akaweza Mtume (saw) kusimamisha Dola ya mwanzo ya Kiislamu katika mji wa Madinah na kuweza kuutoa Uislamu kutoka kuwa kama ujumbe wa kinadharia na kuelekeza hali yake asili ya kuwa na utawala unaofanya kazi kivitendo katika hukmu na usimamizi kamili katika nyanja zote za maisha.

Funzo kuu katika tukio hili ni kwamba da'wah ya Mtume (saw) ilikuwa na mipango, mbinu na malengo maalumu ya kusimamaisha utawala utakaobeba mfumo aliokuja nao yaani Uislamu. Aidha, tunapata mazingatio ya kusimama kidete katika ulinganizi kwa msimamo wa subra, umahiri, kumtegemea Allah (swt) pekee bila ya kuteteleka wala kukata tamaa hususan katika utafutaji wa nusra, kwani siri ya jambo hilo ipo mikononi mwa Allah (swt) peke Yake, bali nyoyo zetu zitulie kwa imani kwamba mwishowe Allah (swt) atawapa nusra waja Wake wanaolingania da'wah Yake tukufu.

أَلَا إِنَّ نَصْرَ اللَّهِ قَرِيبٌ

"Jueni kuwa nusura ya Mwenyezi Mungu ipo karibu" [Al-Baqara: 214]

**Masoud Msellem**
**Mwakilishi kwa Vyombo vya Habari Hizb ut-Tahrir Tanzania**



# Njia ya Mtume (saw) Kuleta Mageuzi

# Halaqa 14: Kutafuta Nusra Kutoka Kwa Watu Wenye Nguvu Na Mamlaka

Katika Halaqa hii tutaangalia kutafuta nusra kutoka kwa watu wenye nguvu na mamlaka.

**Kianzio cha Kuchukua Uongozi**

Hakika utafutaji wa Nusra ni katika sehemu muhimu, na ni katika matendo ya hatari ambayo yanabebwa na da'wah; na wanakuwa na majukumu makubwa wale waliosimama na hili jambo, kwa vile wanavyojitolea kwa kiasi kikubwa. Kukubali kwao kuwa watu wa nusra, wameuza roho zao kwa ajili ya Allah, na wakabeba roho zao katika vitengele vyao ili waende Jannah/peponi…! Na hakika kutafuta Nusra ni amri kutoka kwa Allah (swt), nayo ni Taklif kutoka kwake Subhaanahu, inatakiwa iwe na usiri wa hali ya juu, haifai mtu yeyote ajue isipokuwa viongozi pekee.

Na inatakiwa kufanywa kwa njia ya ukamilifu, na ifahamike kuwa hii ni sehemu muhimu ambayo haiwezi kutenganishwa na twariqa ya kubeba da'wah. Haijuzu kwetu kujisahaulisha ama kuiruka ama kushika njia nyengine, na hii yafanana na amali yoyote katika amali za faradhi alizofaradhisha Allah Azza wa Jalla. Kwa hiyo kutafuta Nusra katika da'wah ni mfano wa kusujudu katika swala, sawa kwa sawa, zote zinatimiza faradhi.

Kwa hiyo Rasul (saw) alikuwa na pupa ya hali ya juu katika kutafuta Nusra, akawa Rehma na Amani zimwendee anakwenda peke yake, ama na mmoja wa maswahaba zake akitafuta Nusra kutoka kwa makabila ili wamkubali/wamwamini na wamnusuru kwa waliomfanyia uadui katika jamaa zake na wamzuie na maudhi. Na alikuwa haendi na mtu ila aliyemuamini na anayeficha siri katika maswahaba wake radhi za allah ziwaendee.

Maqureysh wakazidisha maudhi kwa Mtume (saw) na kwa maswahaba zake mpaka wakadhikika, na hakukubakia matarajio ya kunusuriwa na makabila baada ya kukataliwa na Thaqif kutoka Twaif kwa majibu mabaya. Na baada ya kukataliwa na Bani Kinda, na Bani Kalbi, na Bani amir bin Swa'swa', na Banu Hanifah, Mtume (saw) alipojitambulisha kwao katika msimu wa Hijja, na hakukubakia tamaa kuwa kuna atakayeongoka katika Maqureysh na kuingia katika Uislamu! Na walipoona Muhammad ametengwa, wakazidi kumpa nyongo, Rasul (saw) akaona ukavu wa watu wa Makkah na kuwa mgumu mujtama'h wa Makkah mbele ya da'wah.

Na masiku yakasonga, na Mtume (saw) anazidi kutengwa, na Maqureysh wanazidi chuki dhidi yake, na watu wanazidi kumpa nyongo...! Mtume (saw) pamoja na hayo yote aliendelea kuwa na thiqa juu ya Nusra ya Allah, yeye pamoja na maswahaba zake, Na kuwa Allah atainyanyua dini yake juu ya dini zote, na sisi tuna kiigizo chema katika misimamo mitatu kutoka kwa Mtume (saw) wakati akijitambulisha kwa makabila akitafuta Nusra tutaitaja katika halaqa hii ila twataraji kuelezea kwa ufafanuzi katika halaqat zijazo. In Shaa Allah:

Kwanza: Wakati anajitambulisha (saw) kwa Bani Shiban bin Tha'alaba.

Pili: Wakati anajitambulisha (saw) kwa Thaqif.

Tatu: Wakati anajitambulisha (saw) kwa Bani Amir bin Swa'swa'

**Itaendelea katika UQAB Toleo 19…In Shaa Allah.**

Endelea Uk..12

# SWALI / JAWABU:
## Trump Kujitoa katika Makubaliano ya Nuklia

**Swali**

Twajua kwamba Amerika ni nchi inayoendeshwa na taasisi na kwamba mtizamo wa Amerika kiulimwengu unasimamiwa na taasisi za utawala ndani ya Amerika, na sio rais. Tunawezaje kuelezea uidhinishaji wa makubaliano ya kinuklia na Iran na kuyaita kuwa ni ushindi, na hivi sasa Trump anajitoa kutoka katika makubaliano hayo na kuyaita maamuzi hayo kuwa ni ushindi? Tafadhali fafanua hili, na pokea shukrani zangu.

**Jibu**

Ni kweli mtizamo wa Amerika kisiasa ulimwenguni unasimamiwa na taasisi na sio rais kibinafsi, japo mbinu za rais hutumika zaidi katika kutoa maamuzi, lakini ambalo halikuulizwa katika swali ni msingi upi unaotoa muongozo kufanya maamuzi hayo ambalo lingetoa jibu kwa swali hilo. Msingi wa taasisi za dola ni maslahi ya Amerika. Lau, katika hali fulani, makubaliano yanahitajika, taasisi hupitisha makubaliano na rais huidhinisha makubaliano. Lau maslahi ya Amerika yanahitaji kufutilia mbali makubaliano, taasisi hupitisha kufutilia mbali na rais huidhinisha kufutilia mbali huko.

Kwa mfano,

1- Iran ilikuwa na umuhimu na kuhitajika kuumakinisha utawala wa kidhalimu wa Bashar, ambaye ni kibaraka wa Amerika, mpaka pale Amerika itakapopata mbadala wake. Amerika iliogopa umaarufu wa mavuguvu ndani ya Syria yaliyokuwa yamenyanyua miito ya Uislamu na hukm ya Kiislamu, iliogopa kuwa dhalimu wao angeangushwa na hivyo utawala wa Kiislamu ungesimama Syria na ushawishi wa Amerika ungeondoshwa katika eneo hilo hususan kasi ya mavuguvugu maarufu ilipozidi ndani ya mwaka 2015 na kuendelea kusonga mbele kutoka sehemu hadi sehemu. Hivyo basi, iliiondoshea Iran vikwazo na kuipa majukumu na kuiwezesha kutekeleza majukumu hayo.
Kwa hiyo ilikuwa ni maslahi ya Amerika kutia saini makubaliano ili kuiondoshea Iran vikwazo mbele yake. Ilikuwa ni makubaliano ya kufedheheswa Iran kwa kila nyanja. Linalodhihirisha hilo zaidi ni yaliyofuata utiaji saini wa makubaliano wa 14/7/2015, ambapo Rais wa Amerika Barack Obama alitoa hotuba iliyopeperusha moja kwa moja na kusema:

*Kuhusiana na makubaliano "njia zote zinazoelekea katika silaha ya nuklia zimekatwa" … Itailazimisha Iran "kuondosha thuluthi mbili za vizalisha nuklia na kuihifadhi chini ya usimamizi wa kimataifa"
* Itaondosha asilimia 98 ya madini ya uranium yaliyo wezeshwa.
* Itakubali vikwazo kurudishwa punde tu makubaliano yakikiukwa
*Daima kukipatia Kitengo cha Kimataifa cha Kawi ya Atom kuweza "kuzuru wakati wowote ambapo kitakapohitaji" (BBC 14/7/2015)

Tumeelezea lengo la Amerika kuhusiana na makubaliano ya nuklia na Iran katika Jibu la Swali la 22/7/2015 baada ya Baraza la Usalama kuyapitisha makubaliano hayo 20/7/2015 tukasema:

"Yote haya yanaashiria kwamba lengo la Amerika juu ya makubaliano hayo ilikuwa ni kuifanyia wepesi na kuiwesha Iran kupitia kuiondoshea vikwazo na kuipa mahusiano ya wazi ili iweze kuendelea na jukumu litakaloipa wepesi kazi ya Amerika na kuipunguzia mzigo na kuipa pumzi juu ya michezo yake dhidi ya serikali na watu wa eneo hilo. Hivyo basli Iran itaendelea kutekeleza sera ya Amerika kivitendo kuhusiana na kadhia ya Iraq, Syria na Yemen hata hivyo licha ya kuwa hayo yangetekelezwa nyuma ya pazia ili kuyaficha yasionekane kama ilivyokuwa awali (kabla makubaliano), hivi sasa yatafanyika peupe nyuma ya pazia inayoonyesha ndani au bila hata pazia!"

Hakika, Iran imecheza dori chafu na ya kihalifu ya Amerika ndani ya nchi hizi ndani ya Syria, Iraq na Yemen, na ilikuwa maarufu na wazi chini ya miito ya kirongo ya kupinga na chini ya kuchochea chuki za kidini.

Kwa hiyo, ilikuwa katika maslahi ya Amerika kuingia katika makubaliano hayo ili kuweza kuunusuru uchumi wa Iran na kuiwezesha kutekeleza kwa kikamilifu mipango ya Amerika katika eneo hilo na kwa kushajiishwa kuwa vikwazo dhidi yake vitaondolewa hususan katika hali ya Syria ambayo ilikuwa inakaribia kutoka katika ushawishi wa Amerika kutokana na udhaifu wa utawala wa dhalimu Bashar. Hivyo basi, dori ambayo Iran ilitakiwa kutekeleza kwa ukamilifu ni kumlinda na huku nayo ikipewa ahadi ya kuondolewa vikwazo. Hali ya Bashar ndani ya mwaka 2015 ilikuwa mbaya mno na alikaribia kupenduliwa, kwa hiyo Amerika ikaingia katika makubaliano na Iran ili kuipa idhini rasmi katika dori ya Syria 14/7/2015. Na ilikuwa si hayo tu, bali pia ilileta jeshi la Urusi baada ya Obama kukutana na Putin 30/09/2015 na kuipa Urusi idhini ya kuingia ili kuunusuru utawala wa Bashar usipinduliwe mpaka pale Amerika itakapopata kibaraka mpya.

2- Lakini mtizamo wa Amerika umebadilika sasa kutokana na kuwa hali ya Bashar sasa iko juu. Hili limetengeneza mtizamo mpya kwa utawala wa Trump, hususan kutokana na yaliyopatikana na Amerika moja kwa moja au kinyume chake ndani ya Iraq na Syria dhidi

*Endelea Uk..13*

ya watu wa nchi hizo zinazohitaji mapinduzi. Kwa hiyo hawahitaji tena kuipa Iran dori yoyote ya moja kwa moja kwa kuwa hali sasa imebadilika, iliyoanza mwisho mwa utawala wa Obama baada ya kuzipa majukumu ya moja kwa moja tawala za Uturuki na Saudi Arabia.

Ukhaini wao dhidi ya mapinduzi ya Syria yaliyokuwa mabaya zaidi ya silaha za Urusi, Iran na washirika wake na utawala wa Syria, ambao ulidhoofisha mapinduzi, lakini utawala wa Uturuki na ule wa Saudi Arabia ulifaulu kupata ushindi kwa niaba ya utawala wa Syria kwa njia za uovu, ambazo ziliipelekea Iran kurudi nyuma kimajukumu kinyume na awali ilivyokuwa ikisimamia dori hiyo kabla Uturuki na Saudi Arabia… Hivyo basi, Amerika ikaifanya jukumu la Iran kama lakuongeza nguvu kinyume na kuwa mstari wa mbele, hali hii iko wazi kwa mujibu wa makubaliano ya Astana. Na hivyo walifaulu kuyasitisha mapinduzi ya Syria kwa kisingizio cha kusitisha kuzidi mauaji. Hii ni moja ya sababu ya Amerika kutangaza kujitoa katika makubaliano ya nuklia na Iran, ambapo maslahi ya Amerika yanaitaka kujitoa katika makubaliano kwa maandalizi ya masharti mapya ili kupunguza dori ya Iran ndani ya eneo hilo. Na hili lilimpelekea Trump kudai kuwa Iran imeipiku Amerika katika manufaa yanayotokana na makubaliano ya nuklia, ili kuonyesha kwamba anataka kujitoa kwa sababu makubaliano hayo kwa mujibu wa madai yake, ni kuwa yanaisaidia Iran kupata silaha ya nuklia. Kwa ukamilifu Trump alidai 08/05/2018 ambapo alitangaza kujitoa kutoka katika makubaliano ya nuklia na Iran kupitia hotuba yake iliyopeperushwa alisema kwamba “Ikiwa makubaliano haya yatawachwa yaendelee, hivi karibuni kutakuwa na ushindani wa zana za kinuklia ndani ya Mashariki ya Kati” na “Hakuna kitendo kilichowahi kufanywa na utawala huo na kilichokuwa hatari zaidi kuliko kile cha azma yake ya utengenezaji wa silaha za nuklia” akaendelea:

“Kinadharia, kile kinachoitwa “makubaliano ya Iran” yalikuwa ni kuilinda Marekani na washirika wetu…makubaliano hayo yaliiruhusu Iran kuendelea kuzalisha madini ya uranium.” Akasema pia: “Viongozi wa Iran kiasili watasema kuwa wanakataa kuzungumzia tena makubaliano mapya; wakiwa tayari kuzungumza, mimi niko tayari, nimejiandaa na naweza” na akasema: “tumewasiliana kwa kirefu na washirika wetu ulimwengu mzima… Baada ya mashauriano hayo, imekuwa wazi kwangu kuwa hatuwezi kusitisha bomu la kinuklia la Iran.” “Hivyo basi, leo natangaza kuwa Amerika imejitoa katika makubaliano ya nuklia na Iran”. “Makubaliano hayo hayasaidii kuilazimisha Iran kusitisha vitendo vyake… Muda mfupi ujao, nitaweka saini uamuzi wa urais kuanza kuvirudisha vikwazo vya Amerika vya kinuklia dhidi ya utawala wa Iran.”

Akaenda na kutia saini maamuzi ya urais na kusema: “Makubaliano hayakujadiliwa vyema…Makubaliano ya Iran ni mabaya tokea mwanzo. Vipengee vya makubaliano hayo havikubaliki kamwe. Tukitoka katika makubaliano ya Iran, tutanndelea kufanya kazi na washirika wetu ili kupata suluhisho la kweli, la kina na la kudumu kuhusiana na vitisho vya Iran…kutokana na makubaliano haya yanayotisha tuliyopewa na utawala huo na ni utawala uliojaa vitisho na mabilioni ya dolari. (Sputnik, Al-Jazeera 8/5/2018)

Hapa iko wazi zaidi kuwa Trump alitaka kutamka kauli za uongo na kudanganya zaidi kuhusu uwezo wa Iran ili kukinaisha sababu za kujitoa kutoka katika makubaliano nao ya kinuklia bila kuelezea sababu za kweli; ambazo ni kuwa maslahi ya Amerika hivi sasa yanaitaka wapunguze dori ya Iran nchini Syria na katika eneo hilo lakini ibakie kuwa tayari kutekeleza yale yatakayohitajiwa na Amerika. Hili linarudiwa na sera ya Amerika, ambayo inabadilisha sera zake kwa mujibu wa maslahi, mfano ilivyokuwa Urusi baada ya mkutano wa Obama na Putin 30/09/2015 na kumpa idhini aingie Syria kumsaidia Iran katika lengo la kummakinisha Bashar. Lakini Urusi ilipojaribu kudandia jukumu lake na kujifanya kama ambaye inafanyakazi kibinafsi kando na ushawishi wa Amerika, maslahi ya Amerika yaliitaka “kuiadhibu” Urusi ili kuikumbusha dori yake na uwezo wake, ndiyo ikapiga mashambulizi ya kijeshi nchini Syriai!

Kama tulivyoonesha katika Jibu kwa Swali la 14/04/2018, “… Mashambulizi ya Amerika yalikuwa zaidi kuiadhibu Urusi kuliko kushambulia silaha za kemikali za Syria. Takriban maeneo kumi yalishambuliwa alfajiri leo.

Hata hivyo maoni ya wajuzi wa kijeshi katika vyombo vya habari asubuhi hii machache katika hayo maeneo ni ya kemikali au vituo vya utafiti, lakini mengi ni ya kijeshi.”Kwa hivyo, Amerika kubadilisha sera yake kwa mujibu wa maslahi ni jambo linalojulikana vyema.

3- Jambo jengine ambalo maslahi ya Amerika yalitaka, ni Amerika kuondosha kuangaziwa kwa uhalifu wa Mayahudi kwa kuvamia Palestina na Al-Quds (Jerusalem), na kwa muda mrefu Amerika ilikuwa ikitaka kuuhamisha ubalozi wao kuupeleka Jerusalem, lakini ilikuwa inasubiri suluhisho la dola-mbili na kugawanywa kwa Jerusalem, na ilikuwa ikihairisha uhamishaji huo wa ubalozi. Lakini sasa Amerika inaona suluhisho tofauti kwa tatizo hilo kinyume na suluhisho la dola-mbili, kwa kuingiza mabadiliko na suluhisho nyingine ambazo wanasema ni makubaliano ya karne hii. Na hili lilihitaji lile lililoidhinishwa na tawala zilizotangulia za Amerika za kuuhamisha ubalozi kwenda Al-Quds (Jerusalem), na Amerika ilitaka kupunguza kuangaziwa kuhusiana na suala hilo na hivyo ikailenga Iran na kulikuza suala la dori yake kwa kuandaa kongamano la watawala (ruwayibidha) 21/05/2017 ambapo Trump aliwazungumzia viongozi hao na wawakilishi wa dola 55 kutoka katika ulimwengu wa Kiislamu ili kuelezea sababu za kutia saini maridhiano kati ya umbile la Kiyahudi na utawala wa Saudi na tawala nyingine na kuendelea kushinikiza

*Endelea Uk..14*

suluhisho fulani kuhusiana na suala la Palestina ambalo lilikuwa halija tangazwa na Amerika. Na utawala wa Saudi unalipigia debe na kuushinikiza Utawala wa Palestina kuukubali, ikimaanisha kuwa Trump aliwekeza kazi yake kuifanya Iran kuwa ndiyo adui badala ya umbile la Kiyahudi mnyakuzi wa Palestina, ardhi ya Isra na M'iraj. Hivyo basi, Saudi Arabia inamfuata Trump unyounyo na kumuunga mkono na kuupigia debe uamuzi wake… Kwa hiyo ni kwa maslahi ya Amerika kuzidisha uongo kwa suala la makubaliano ya nuklia, kama ambaye sio makubaliano yanayo ifedhehesha Iran, lakini ni makubaliano yanayoia nguvu Iran. Muhimu zaidi ni kuwa makubaliano yaliyokuwemo ndani, hata Trump na wengine hawatopata makubaliano zaidi ya hayo ya kuifedhehesha Iran.

Imeoneshwa kuwa Amerika inailenga Iran kuionyesha kama adui ndani ya eneo hilo badala ya umbile la Kiyahudi. Kwa mfano maandamano ya hivi majuzi ndani ya Iran, Amerika iliyazingatia maandamano hayo na ikayadandia ikizingatia dori ya Iran katika eneo hilo ni suala ambalo Amerika inalipa makini katika sera yake. Na Amerika kudandia wimbi hilo la maandamano ndani ya Iran hakukulenga kuupindua utawala huo bali kwa malengo mengine tuliyoelezea katika Jibu kwa Swali la 11/01/2018:

"...Kwa nini Amerika ilidandia wimbi la maandamano na kulitumia vipi? Ilikuwa ni kwa sababu mbili:

Kwanza ilikuwa kuondosha kuangaziwa kwa Palestina na kauli ya Trump kuhusu Al-Quds "Jerusalem" na kulishughulisha eneo hilo na suala la Iran. Hivyo, ikawa adui wa kwanza katika eneo na kisha kuangaziwa kunaelekezwa Iran, na huku umbile la Kiyahudi mnyakuzi wa Palestina linasita kuangaziwa.

Pili ni kuwamakinisha vibaraka wa Amerika katika eneo hilo chini ya kisingizio cha kuungana dhidi Iran na kuilinda Amerika kutoka katika hatari ya Iran. Kauli ya Trump kuhusu Al-Quds (Jerusalem) na kwamba ndiyo mji wa umbile la Kiyahudi (adui mkubwa wa waumini) kama tulivyosema katika toleo 7/12/2017 ni kama kofi katika migongo ya vibaraka wa Amerika "Al-Quds (Jerusalem) imo katika mioyo ya Waislamu na akili zao, na kimya cha vibaraka juu ya kauli ya Trump na kujipendekeza kwao ubakia kuwa vibaraka wa Amerika ni kashfa kwao…Kauli ya Trump dhidi ya Iran ni Kamba yao ili wabakie mamlakani kuwa vibaraka wa Amerika licha ya kauli ya Trump kuhusu Jerusalem… kwa kusema kuwa Trump anaikabili Iran, adui mkubwa ni kujitia hamnazo ambako ni kubaya kuliko uhalifu.

قَاتَلَهُمُ اللَّهُ أَنَّى يُؤْفَكُونَ

"Mwenyezi Mungu awaangamizilie mbali! Vipi wanapotoka na haki?" [Al-Munafiqun: 4]

4- Amerika ilikuwa nchi yenye ushawishi katika makubaliano ya nuklia, Ulaya ilikubali mpango wa Amerika kuhusiana na makubaliano na kukubali tu kutia saini kwa kuwa ni mmoja katika watiaji saini. Hivyo, Ulaya ilijisalimisha na kukubali ili kuweza kuendelea kuwepo. Tulifafanua nafasi ya Ulaya katika makubaliano ya nuklia katika Jibu kwa Swali la 22/07/2015 na tulisema wakati huo:

"...Kwa kuwa hakukua na chochote kilichobakia kwa Ulaya, baada ya kutafakari kuwa hawawezi kusitisha makubaliano ya nuklia kati ya Amerika na Iran au kuweza kuwa na ushawishi juu ya Amerika isipokuwa kuelekea Iran kwenda kupata ngawira kwa njia ya kujishindia uwekezaji na miradi ndani yake, kwani (Ujerumani) inaumia kutokana na matatizo ya kiuchumi na kupitia hali hiyo wanaweza kufanyakazi ndani ya Iran kwa muda mrefu ili kuweza kupata tena ushawishi wa Ulaya ndani au japo kidogo ikiwa pamoja na ushawishi wa Amerika…"

Hivyo basi, Ulaya waliyatumia makubaliano hayo na kujifungua kwa Iran kiuchumi. Mgao wa biashara kati ya Ulaya na Iran umezidi na biashara kati ya Amerika umepungua kidogo kabla ya makubaliano na wakati wa vikwazo. Hiyo ilikuwa sababu ya tatu ambayo ilimfanya Trump kwenda mbio kuyasitisha makubaliano hayo ili kuipiga pigo Ulaya kibiashara… Trump alitangaza 7 Mei 2018 kupitia tweet katika mtandao wa Twitter kwamba ameamua kuileta karibu tarehe ya makubaliano ya nuklia ya Iran kutoka 12 hadi 8 Mei 2018.

Ni muhimu kuangazia kuwa hatua hii imekuja kwa sababu Ulaya ilijaribu kumnasihi asijitoe katika makubaliano ya nuklia. Tovuti ya "Al-Arabi Al-Jadeed" ili nukuu, موقع إكسيوس alalam.ir tovuti kwamba "… Katibu wa Masuala ya Nje wa Amerika, Mike Pompeo aliwaambia wenzie kutoka Ulaya, Ufaransa, Uingereza na Ujerumani siku ya Ijumaa 4/5/2018 kuhusu nia ya Rais Trump kutangaza kujitoa kwa nchi yake kutoka kwenye makubaliano ya nuklia, na alikataa maelewano yaliyopendekezwa na wawakilishi wa Amerika ndani ya miezi iliyopita kuhusu uwezekano wa kufanya mabadiliko ya makubaliano" Amerika haikukubali kuelewa wala kushirikiana pamoja na Ulaya na haikuwajali na hii inaashiria kuwa ina mipango mingine na inataka kujitenga na Ulaya na kutoshirikiana nayo katika suala hili.

5- Ulaya imegundua kuwa kusitishwa kwa makubaliano itawapa madhara makubwa ya kiuchumi ikiwapelekea katika madhara ya kisiasa na hivyo basi wamejaribu juhudi zao zote kukutana na Trump kumrai asijitoe. Macron alikwenda Amerika na kujaribu kumrai rais wa Amerika asijitoe kutoka katika makubaliano hayo lakini hakufaulu. Akafuatiwa na Merkel, na wakatoa mapendekezo ya kibiashara kwa Amerika lakini hayaku kubaliwa. Nafasi ya Ulaya iliibuka kuwa ya udhaifu. Uingereza ikawasiliana na Macron na Merkel, na kutangaza kuwa wao watabakia katika makubaliano ya nuklia na Iran. Kisha, Waziri wa Kigeni wa Uingereza, Johnson, akazuru Amerika na kutangaza kuwa ulimwengu upo salama zaidi kwa kubakia makubaliano kuliko bila. Uingereza ikaanza kusonga mbele

***Endelea Uk..15***

kwa nguvu. Hivyo basi, Trump akaisogeza tarehe ili kuonyesha nafasi yake katika makubaliano hayo kutoka tarehe 12 hadi 8 Mei 2018 na kuusitisha mipango ya Ulaya na kutangaza rasmi na hakuipa uzito Ulaya kwa sababu taasisi za Amerika ziliona dhamira yao kupitia sababu hizo tatu kwa Amerika kusitisha makubaliano.

6- Yaliyofuata yalikuwa kama ifuatavyo:

a. Ulaya imesikitishwa, imejaa majuto na wasiwasi! Chansela wa Ujerumani Angela Merkel alisema alipokea taarifa hiyo kwa majuto na wasiwasi juu ya uamuzi wa Rais wa Donald kuitoa Amerika katika makubaliano makubwa ya kinuklia na Iran ya mwaka 2015. Alisema "Tutaendelea kujifunga na makubaliano haya na tutafanya kila tuwezalo ili kuhakikisha kuwa Iran inayatekeleza kiukamilifu. Ujerumani imechukua uamuzi huu kwa ushirikiano na Uingereza na Ufaransa," akaongeza. "Suluhisho lipo katika kuzungumza kwa pamoja na kwamba Ulaya inatakiwa kucheza dori kubwa zaidi katika sera ya kigeni na usalama." "Alisisitiza kuwa Ujerumani itafanya kila iwezalo ndani ya uwezo wake kuhakikisha Tehran inatekeleza majukumu yake vilivyo chini ya makubaliano ya nuklia na ikaashiria kuwa Tehran imekuwa ikiyatekeleza hadi sasa na kusema kuwa makubaliano ya nuklia ya Iran yasiulizwe maswali bali kuweko na mazungumzo kuhusu makubaliano ya kina zaidi ya kwenda zaidi ya makubaliano ya mwanzo." (Reuters, 9/5/2018).

Alitangaza kuwa Ulaya imehuzunishwa na Amerika kufeli na wasiwasi wake kuhusu athari ya kujitoa huko kutoka katika makubaliano. Kama tulivyosema huko juu kuwa Ulaya ili kwenda mbio katika ngazi za juu za Amerika kuhakikisha wanamrai Trump asifanye maamuzi ya kujitoa na kujaribu kumpendekezeaTrump ajadiliane na Iran tena, lakini hakuwajibu bali aliwashtusha kwa tarehe ya kutangaza msimamo wake juu ya makubaliano hayo. Hivyo basi, Ulaya walionyesha udhaifu mbele ya Amerika.

Kisha, wiki ya pili ya Mei 2018, kulikuwepo na kauli kinzani zikidhihirisha kutoridhishwa na kutamaushwa kwao na kujitoa kwa Amerika. Kwa upande mwingine baadhi ya kauli zilizotolewa zilionyesha hali ya changamoto, Federica Mogherini, kiongozi mkuu wa sera ya Umoja wa Ulaya, alisema "Nina wasiwasi kuhusiana na tangazo hili litakalotolewa na Trump." Akiongeza, "Umoja wa Ulaya umejizatiti kutenda kwa mujibu wa maslahi yake ya kiusalama ili kulinda uwekezaji wake wa kiuchumi"… Tutabakia ndani ya makubaliano haya kwa ushirikiano na jamii ya kimataifa." Majibu ya Waziri wa Kigeni wa Ufaransa, Jean-Yves Le Drian alisema: " Bado makubaliano hayaja kufa…Ufaransa, Ujerumani na Iran itafanya mkutano Jumatatu (14/5/2018) ili kujadili matukio haya mapya na zana za Iran za masafa marefu na masuala mengine, lakini wakati huo huo lazima tuyabakishe makubaliano, nasisitiza kuwa Kitengo cha Kimataifa cha Kawi ya Atom kinakiri kuwa Iran inaheshimu makubaliano" (Al-Jazeera 9/5/2018).

Uingereza, Ufaransa na Ujerumani zilitoa taarifa ya pamoja ikionyesha kuungana kwao: "Pamoja tunasisitiza kuendelea kwetu na makubaliano ya JCPOA. Tunazinasihi pande zote kubakia na kujifunga na utekelezwaji wake kikamilifu na kutenda majukumu yanayowahusu, ikiwa ni pamoja na kuhakikisha kuendeleza manufaa ya kiuchumi yanayohusiana na makubaliano ya watu wa Iran." (Al-Jazeera 9/5/2018).

"Maamuzi ya Washington kujitoa kutoka katika makubaliano ya nuklia hakubadilishi msimamo wetu na hatuna nia ya kujitoa," Johnson alisema hayo ndani ya bunge la nchi yao. "Nainasihi Marekani kujiepusha na kitendo chochote kitakachositisha pande nyingine kuendelea na utekelezwaji wa makubaliano hayo, ikiwa ni pamoja na maslahi yetu ya pamoja ya kiusalama." (Guardian 9/5/2018). Misimamo hiyo inaonyesha kuwa Ulaya itakuwa kikwazo na itabakia kuyaunga mkono makubaliano!

Kwa upande mwingine, baadhi ya kauli za Ulaya zilionyesha kuwa wamesalimu amri na kuwa na wasiwasi na makampuni yao. "Itakuwa vigumu kutekeleza makubaliano ya nuklia bila Amerika," alisema Norbert Roitgen, kiongozi wa sera ya kimataifa ndani ya chama cha Merkel. Norbert akaongeza kuwa yeyote "atakayewekeza nchini Iran atakuwa na vikwazo vikali kutoka kwa Amerika, na bei yake itakuwa haiwezi kulipika." Akaonya kwa kusema "Hivyo basi, makampuni yaliyoathirika kwa haraka yatasitisha uwekezaji au kujitoa kutoka nchini humo moja kwa moja." (Der Spiegel, Ujerumani, 9/5/2018).

Waziri wa Kigeni wa Ufaransa Jean-Yves Le Drian, alisema tarehe 9/5/2018 kupitia Channel ya RTL kwamba: "Iran ilikuwa imekubali kujiwekea vikwazo katika mipago yake ya kinuklia ili waweze kupata manufaa ya kiuchumi ambayo Ulaya ilijitahidi kuhifadhi. Na kwamba usimamizi wao utakutana na makampuni ya Kifaransa yanayo fanya shughuli zake nchini Irani ndani ya masiku kadhaa kujadiliana ni namna gani tunaweza kuwasaidia kubakia nchini Iran na kujaribu kuwalinda kwa hali yoyote ile kutokana na vitendo vya Amerika," na hivyo basi Ulaya ilidhihirisha wasiwasi kuhusu hali yao ya kiuchumi.

b- Msimamo wa Iran kwa kiasi fulani ulikuwa wa utulivu, na haukuegemea Ulaya. Rais wa Iran Hassan Rouhan aliyaelezea maamuzi ya Trump kama "vita vya kifikra na ushinikizaji wa kiuchumi." Alisema, "Hatutomruhusu Trump kushinda vita vya kifikra na kuwashinikiza watu wa Iran kiuchumi," akasema, "Nchi hii itabakia kujifunga na makubaliano ya nuklia bila Amerika, kwa sharti kuwa Iran ndani ya wiki kadhaa itapata uungwaji mkono kutakako tuwezesha kupata manufaa kamili ya makubaliano hayo kwa kupata dhamana kutoka kwa washirika

Endelea Uk..16

waliobakia wa makubaliano hayo ya nuklia ambao tumo katika mazungumzo nao. Suala lote litategemea dhamana ya maslahi yetu ikiwa yatapata uungwaji mkono tutaendelea na makubaliano hayo, lakini ikiwa dhamana itakuwa katika karatasi tu na hayadhamini maslahi ya watu wa Iran basi tutakuwa na uamuzi kamili." (Runinga rasmi ya Iran 9/5/2018).

Spika wa Baraza la Shura la Iran, Ali Larijani alisema: "Ulaya imejisalimisha kwa shinikizo za Amerika ambayo imepelekea kujitoa kwa makampuni yao mengi ndani ya Iran kwa mujibu wa vikwazo vya kimataifa vilivyotangulia kati ya 2012 na 2015… Hatuwezi kuzipa uzito kauli zao za kuendelea na makubaliano, lakini inafaa kutoa mtihani kwa wiki kadhaa ili tuweke wazi kwa ulimwengu kuwa Iran imejaribu kwa kila njia kufikia suluhisho la kisiasa kwa Amani." (Deutsche Welle, 9/5/2018) Iran haina ujasiri na msimamo wa Ulaya, ina wasiwasi kuhusiana na maslahi yake na lau vikwazo vitawekwa basi itadhuriwa.

C –Urusi haikujumuisha msimamo wake dhidi ya Trump na msimamo wa Ulaya, bali ilitoa msimamo wake pekee. "Urusi imesikitishwa na uamuzi wa Trump… hakuna na hakutakuweko na msingi wa kusitisha, makubaliano ambayo yalionyesha kufaulu pakubwa… na kwamba Moscow iko tayari kuendelea na ushirikiano na washirika wengine ndani ya makubaliano hayo ya nuklia na itaendelea kukuza mahusiano yake na Iran." Al Jazeera 9/5/2018)" alisema Waziri wa Kigeni Lavrov.

Na inazungumza kiuoga kuhusu ushirikiano wake na wahusika wengine, yaani pande za Ulaya ambao hawakuwasiliana na Urusi, waliamua kukutana na kushauriana na Iran bila kuwepo kwake. Hivyo basi, msimamo wa Urusi uko katika hali tete, haiwezi kuungana na Amerika katika suala hilo, kwa sababu ni kinyume na maslahi yake na sera yake juu ya Iran na haiwezi kuungana na Ulaya ambao wanaharibu mahusiano yao na Urusi ili isiweze kutumiwa na Amerika dhidi yao katika kuitenga Ulaya.

d- Ama kuhusu msimamo wa Uchina, balozi maalumu wa Uchina katika eneo la Mashariki ya Kati, Gong Xiaosheng alisema: "Pande zote husika katika makubaliano ya nuklia na Iran lazima wayaheshimu na watumie mazungumzo kujadiliana ili kusuluhisha sintofahamu, na nchi yake iko tayari kujumuisha ushirikiano wa nchi zote husika," (Xen-Kho 9/5/ 2018). Hii ni kauli ya wazi isiyokuwa na mwelekeo wa moja kwa moja, ambao Uchina haijaziunga mkono nchi za Ulaya ambazo zinapinga kujitoa katika makubaliano hayo. Lakini imeiweka misimamo ya Amerika na Ulaya kuwa sawa kwa sawa kwa mujibu wa kauli hiyo. Uchina haihesabiwi kutokana na udhaifu wa msimamo wake kimataifa dhidi ya Amerika na imejifunga na uhusiano wake kibiashara na Amerika.

Kwa kutamatisha: Trump hakutangaza kujitoa katika makubaliano kwa sababu makubaliano hayo eti yalikuwa ni ushindi kwa Iran na kwa maslahi ya Iran na kuikuza hadhi ya Iran, lakini kwa mujibu wa makubaliano yalivyo tangu wakati wa Obama ni kufedheheshwa kwa Iran kutokana na kukubali kwake kusitisha mradi wake wa nuklia. Lakini Trump alitangaza kujitoa kutoka katika makubaliano kwa sababu maslahi ya Amerika yameitaka kufanya hivyo kwa mujibu wa nukta tatu tulizozitaja hapo juu:

A – Umuhimu wa dori ya Iran, hususan ndani ya mwaka 2015. Hili halihitajiki tena kama ilivyokuwa mwaka 2015.
B – Kuzidisha chuki ya Amerika dhidi ya Iran, hususan mbele ya Saudi Arabia na mfano wake ili kuzihamisha chuki dhidi ya umbile la Kiyahudi na kuzipeleka kwa Iran…
C- Kuiadhibu Ulaya, hususan kibiashara kwa sababu Ulaya ilipatiliza makubaliano hayo kwa kufungua biashara na Iran na kusitisha mahusiano ya kibiashara na Amerika.

Amerika na Magharibi, kama waliowatangulia, makafiri na washirikina, hawa heshimu ahadi na hawatimizi mikataba, lakini wana vunja ahadi na mikataba kila wakati na hawaogopi. Iko wapi thamani ya Uislamu na hukm zake zinazotulazimu kutimiza mikataba na makubaliano? Mwenyezi Mungu alisema:

**يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا أَوْفُوا بِالْعُقُودِ**

"Enyi mlioamini! Timizeni ahadi" [Al-Ma'ida: 1].

Kwa kweli wanadamu leo wanahitaji dola ya Khilafah Rashida kwa njia ya Utume, baada ya Makafiri kueneza ufisadi katika ardhi, kuwadhulumu watu na kuharibu kila kilicho na kisichokuwa na uhai. Dola itakayo tekeleza mikataba na kuhifadhi ahadi na kueneza uadilifu na usalama kati ya watu…

Waislamu watanyanyuka kwa kuisimamisha, kwa kutokana na utukufu, ushindi na mwamko wake, na ukweli ni ule ambao Mtume (saw) aliusema aliposema kuielezea Khilafah kama ngao ya Ummah kutoka katika majanga, udhaifu na udhalili:

**«إِنَّمَا الْإِمَامُ جُنَّةٌ يُقَاتَلُ مِنْ وَرَائِهِ وَيُتَّقَى بِهِ»**

"Imam ni ngao nyuma yake mnapigana na kujihifadhi." [Ilivyosimuliwa na Muslim kutoka kwa Abu Hurayrah (ra)]

**27 Sha'ban 1439 H**
**13/5/2018 M**